



Hongera! Sasa umekua mkandarasi na unaruhusiwa kufanya miradi yenyeye thamani isiyozidi kiwango cha ukomo wa daraja lako. Kama Mkandarasi, Bodi inapenda ufahamu na kuzingatia mambo yafuatayo;

Ili kujihakikisha kwamba unafahamu kila kinachoendelea katika biashara ya ukandarasi, pamoja na mambo mengine, ni vizuri kuhakikisha unapata taarifa zote kutoka Bodi yako ya Usajili. Unashauriwa kujenga mazoea ya kutembelea tovuti ya Bodi, www.crb.go.tz na kila inapoweze kana, kutembelea ofisi za Bodi popote ambapo utapata taarifa kupitia watumishi wa Bodi au mbao za matangazo katika ofisi husika. Pia hakikisha unasoma kijarida cha Bodi, "The Contractor" kinachotolewa kila robo ya mwaka.

<p>Mfuko wa kusaidia Makandarasi (Contractors Assistance Fund CAF); Unayo fursa kuwa mwanachama wa mfuko wa kusaidia makandarasi utakaokusaidia kupata dhamana za benki kwa ajili ya zabuni na malipo ya awali. Ili kuwa mwanachama, jaza fomu ya maombi. kwa maelezo zaidi tembelea tovuti ya Bodi.</p>	<p>Kulipa ada ya mwaka; Lipa ada ya mwaka kwa wakati. Taarifa ya madai hutumwa kwa Makandarasi wote kila mwezi Julai. Hakikisha kila wakati hudaiwi ada. Kutolipa ada kutasababisha kufutiwa usajili. Unaweza pia kutembelea ofisi za Bodi kujua kama unadaiwa ada.</p>
<p>Dispensation; Kupitia utaratibu wa 'dispensation' utaruhsija kufanya mradi wenye thamani zaidi ya ukomo wa daraja lako lakini usiozidi kikomo cha daraja la juu yako. Utatakiwa kujaza fomu ya maombi. Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti ya Bodi.</p>	<p>Kusajili Mradi; Kila upatapo mradi wa thamani ya TZS 10 milioni na kuendelea, hakikisha umeusajili kwa Bodi na kubandika stika katika bango la mradi. Kutosajili mradi na/au kutobandika stika ni kosa kisheria. Jaza fomu ya maombi kusajili mradi. Tembelea tovuti ya Bodi kujua utaratibu wa kusajili mradi.</p>
<p>Ubia (Joint Ventureship - JV); Kupitia utaratibu wa ubia, unaweza kuijunga na makandarasi wenzako na kuruhusiwa kuomba zabuni na kutekeleza mradi wenye thamani inayozidi ukomo wa daraja lako. Unajaza fomu ya maombi. Tembelea tovuti ya Bodi kwa maelezo zaidi.</p>	<p>Kuwasilisha fomu za mwaka za mrejesho kwa mtando; Kila mwisho wa mwaka wa fedha, unakumbushwa kujaza na kuwasilisha kwa njia ya mtando fomu za mwaka za mrejesho. Fomu huwasilishwa kati ya julai hadi septemba ya kila mwaka. kutowasilisha fomu hizo ni kosa kisheria. Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti ya Bodi.</p>
<p>Mafunzo; Kupitia mpango mahsusini wa Bodi wa mafunzo endelevu kwa makandarasi (Sustainable Structured Training Programme - SSTOP), Bodi huendesha mafunzo yenye lengo la kunoa ujuzi wa makandarasi. Hakikisha unahudhuria mafunzo haya kila yanapofanyika katika vituo mbali mbali nchi nzima. Tembelea tovuti ya Bodi kupata ratiba ya mafunzo hayo kwa mwaka mzima.</p>	<p>Utii wa sheria, kanuni na taratibu za ujenzi; Hakikisha unatii sheria zote zinazoongoza biashara ya ukandarasi hapa nchini. Hii ni pamoja na kuhakikisha usalama wa watenda kazi wako na wapita njia.</p>
<p>Semina na Makongamano; e Bodi huendesha semina na makongamano ikiwemo mikutano ya mashauriano (Annual Consultative Meetings - ACMs) kwa lengo la kupeana taarifa na kujadili masuala mbalimbali yahusuyo mazingira ya biashara ya ukandarasi. Hakikisha unahudhuria mikutano hii ili kupata taarifa na uelewa na pia kukutana na makandarasi wenzako na wadau wengine wa sekta ya ujenzi.</p>	<p>Malipo ya adhabu na Faini; Kil inapotokea umevunja sheria za ujenzi na kupewa adhabu na faini, hakikisha unalipa mara moja. Kushindwa kulipa adhabu na faini kutasababisha kufutiwa usajili.</p>

Head Office;

Mkandarasi Place, Plot No. 5
Block "A", NCC Link, First Floor
P.O.Box 96, Dodoma
Tel: +255 - 26 2962403/4,
Email: crbhq@crb.go.tz

Eastern Zone,

Pamba Road, Tetex House, 3rd Floor
P.O.Box. 33621, Dar es salaam
Tel: 255 22 2137962-3
Email: crbez@crb.go.tz

Lake Zone;

Staion Road,Tanroad Compound,
P.O.Box 2815 Mwanza
Tel: +255 - 28- 2500218/2502212
E-mail: crlz@crb.go.tz

Southern Zone;

NHIF Tower 3rd Floor,
P.O.Box 1690 Mbeya
Tel: +255 - 25- 2502480
E-mail: crbsz@crb.go.tz

Nothern Zone;

NSSF Mafao House, 11th Floor, Uzunguni Area
P.O.Box. 16795, Arusha
Tel: +255 - 27 2520167
E-mail: crbnz@crb.go.tz

Central Zone;

Mkandarasi Place, Plot NO.5
Block "A", NCC LINK
Mezzanine Floor
P.O.Box. 2618, Dodoma
Tel: +255 26 2962405 2966040-1
E-mail: crbcz@crb.go.tz